JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI – NJOMBE.

SHULE YA SEKONDARI MBEYELA,
S.L.P 871,
NJOMBE.
30/11/2020.

KUMB.NA: - MBYSS/NTC/JI/14
JINA LA MWANAFUNZI ……
S.L.P ……
NJOMBE.

YAH. MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBEYELA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE, MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.

1. **UTANGULIZI**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya sekondari Mbeyela. Shule hii ipo mjini Njombe mtaa wa SIDO umbali wa km 1 kutoka barabara kuu iendayo Songea, na inamilikiwa na Halmashauri ya Mji Njombe.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. SARE YA SHULE

(a) WAVULANA

(i) Mashati meupe mawili mikono mirefu (yasiyo ya kubana)
(ii) Suluali mbili rangi kaki (aina ya kitambaa kimeambatanishwa) isiyo ya kubanwa
(iii) Masweta mawili rangi ya udongo – "V" – shingoni (aina na rangi imeambatanishwa)
(iv) Viatu vyeusi jozi mbili vyenye gidamu (kamba) na kisigino kifupi
(v) Soksi jozi mbili rangi nyeusi
(vi) Daftari kumi (counter book), mkebe na rula ndefu (sentimita 30) kalamu ya mkaa na kalamu za wino za kutosha.

(b) WASICHANA

(i) Kigauni rangi ya udongo kinachofika magotini (naambatanisha mchoro) vigauni viwili
(ii) Mashati meupe mawili mikono mirefu (yasiyo ya kubana)
(iii) Viatu vyeusi jozi mbili vyenye gidamu (kamba) na kisigino kifupi
(iv) Suluali mbili rangi udongo za heshima ambazo hazibani (aina ya kitambaa kimeambatanishwa)
(v) Masweta mawili rangi ya udongo – "V" – shingoni (aina na rangi imeambatanishwa).

(vi) Soksi jozi mbili rangi nyeupe
(vii) Daftari kumi (counter book), mkebe na rula ndefu (sentimita 30) kalamu ya mkaa na kalamu za wino za kutosha.
(viii) Mahitaji mengine kwa msichana mzazi/mlezi unayafahamu

2.2. CHAKULA

(a) Mahindi yasiyokobolewa debe 2 (40kgs)
(b) Maharage lita 20 (20kgs)
(c) mchele lita 10 (10kgs)
(c) Fedha Tshs 81,000/= (Uboreshaji taaluma 21,000/=, Chakula 60,000/=)
Michango hii ni kwa mwaka mzima.
Fedha hizo ziingizwe **Benki NMB Akaunti Namba 60610003749**Jina la Akaunti **JOSEPH MBEYELA SEKONDARI**. Michango hii ni makubaliano ya wazazi Mbeyela Sekondari na italipwa kwa awamu mbili.
NB: - Kila kimoja nusu kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili utamalizia kiasi kilichobaki.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni: -

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote inapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za umma.
(j) Mwanafunzi haruhusiwi kushinda shule bila ruhusa, na endapo itatokea ameshinda mzazi/mlezi atawajibika kununua roll moja ya waya wa fensi ya shule.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MBEYELA

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……. Tarehe ya kuzaliwa (taja mwaka na mwezi).

2. Kabila …….

3. Dini na dhehebu ……

4. Jina Baba/Mlezi ……

5. Anuani ya Baba/Mlezi ……..

6. Kazi ya Baba/Mlezi ……..

7. Jina la mama ……. Kazi yake ……

8. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana …….

9. (a) Mwanafunzi anaishi na nani? ……
   (b) Kama anaishi na mlezi, sababu za kuishi na mlezi ni zipi? ……

10. Nathibitisha kwamba taarifa zote nilizotoa ni za kweli na sahihi.

    Sahihi ya mwanafunzi …… tarehe ……..

    Sahihi ya mzazi/mlezi ……. Tarehe ……

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

SHULE YA SEKONDARI MBEYELA

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi …… msichana/mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha …… mwaka ……. Katika shule ya sekondari mbeyela na nitafika shuleni bila kuchelewa.

Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za nchi.

Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Sahihi …….. tarehe ……

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.

Mimi …… ninakubali mtoto wangu kuingia shule ya sekondari Mbeyela kidato cha …….. mwaka …….. na ninaahidi kumlipia michango ya shule na kumpatia mahitaji yote muhimukwa wakati kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule (joining instruction) na ninahakikisha kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na taifa.

Anuani yangu ya kudumu: -

……..

……

……

Simu: ……..

Sahihi …… Tarehe ……